

Pambazuko

Toleo Namba 059

Jumatatu Januari 29-Februari 4, 2024

Biashara Ikulu Z'Bar yavuruga uongozi

● Sababu za waziri
'kuachia ngazi' zaanikwa

Uk. 12, 13 & 14



MAELEZO YA
PICHA UK. 3

Ni zamu ya CCM kuandamana Uk. 5

Anayepanga
kuiba kura,
atakufa -
Lema Uk. 6



Habari za Afrika
Mashariki Uk. 11&19



Jicho la Tai

Mpango arejeshe ujira
wa Novemba Uk. 10

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Viongozi wasiongeze adha barabarani

TAARIFA kwamba misafara ya viongozi wakuu wa serikali kusimamisha shughuli za uzalishaji mali katika maeneo wanakopita, siyo ngeni na kamwe siyo uongo.

Watanania wamekuwa mashuhuda wazuri wa kadhia hii ya kusimamishwa kwa saa kadhaa barabarani – baada ya njia kufungwa, wakisubiri mkubwa mmoja apite.

Pamoja na kwamba hatuna lolote kubwa la kuwalalamikia viongozi wa juu; rais, makamu wake, waziri mkuu na Rais wa Zanzibar, wanapokwenda kwenye shughuli na kulazimisha wanausalama kufunga barabara ama kuzuia magari kusogea, lakini tunabeba kilio cha wananchi wengi wanapoona viongozi wengine wakilazimisha njia kufungwa kwa kuwa na wao wanapita.

Imekuwa ni kawaida, kwa miaka ya hivi karibuni wananchi kusimamishwa kwa muda mrefu barabarani ama kufunga shughuli zao kwa kuwa baadhi ya viongozi wa mamlaka na idara kadhaa za serikali wanapita; ama wakienda kazini asubuhi, ama kurudi nyumbani jioni au pengine kwenda kuhudhuria shughuli nyingine.

Hawa ni pamoja na magari ya mawaziri, manaibu wao, wakuu wa idara za usalama na wengine ambao wanakuwa wakiongozwa na magari ama pikipiki za Polisi, kuashiria kuna mkubwa anaongozwa.

Hali hii imekuwa kero, siyo Dar es Salaam tu au kwenye miji mingine mikubwa, bali hata mikoani na wilayani. Kwamba anapopita mkubwa, watu wananyimwa uhuru wao wa kujongea kwenda ama

kutoka kwenye shughuli zao za kusaka maisha ya kila siku, kisa kuna mkubwa anapita.

Sisi tunatambua kuwa Katiba inaamrisha kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, afanye shughuli zake halali bila kubughudhiwa na yeyote, lakini anapozingwa na misafara ya viongozi, hata wale wasiohitaji kuzuia watu kuendelea na shughuli zao, inakuwa kero kubwa na uonevu.

Katika kuzuia watu kusonga, kisa misafara, mbali na kwenda ama kutoka kwenye shughuli zao, pia wapo baadhi ya madereva wanaodai kuwa na wagonjwa – wakitumia magari binafsi, ambao nao kusababisha foleni kubwa kwa kuonesha wanalazimika kuwahi maeneo mahsusi – ikiwamo hospitali kwa ajili ya kuokoa maisha- hii siyo sawa.

Inawezekana Dar es Salaam ndiyo inaongoza kwa kero hiyo, lakini kwanini iwe kwenye jiji hilo tu wakati wakubwa wengi wanatakiwa kuwa makao makuu ya nchi, Dodoma?

Kwanini wakati mwingi wakubwa hao wapo kwenye jiji ambalo wakazi wake wanatakiwa kukimbizana na muda kwenye shughuli za kuzalisha mali ili waweze kulipa kodi na siyo kusimamishwa barabarani?

Sisi katika Pambazuko tunaomba wakubwa wetu kuacha kupoteza muda wa wananchi barabarani, kisa wao wanapita. Kama ni lazima sana wao “kuwahi,” basi Polisi washauri wakubwa hao kuchelewa kidogo kutoka nyumbani ama kuwahi kutoka kazini, ili wasilete kero zaidi ya barabarani kwani foleni zilizopo ni adha ya kutosha.

TUMEKUBALIANA HIVI...



WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba akizungumza na mwenzake wa Sudan Kusini, James Morgan (kulia) ambapo kumefanyika makubaliano ya walimu wa kufunza Kiswahili kupelekwa Sudan Kusini. Mawaziri hao walikutana mwishoni mwa wiki. (Picha na mtandao wa X).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

KUTOKA UK. 1: Mwanaharakati, Dkt. Anania Nkya akiwa na bango linalihimiza kuwepo kwa katiba mpya Tanzania. Alishiriki maandamano yaliyofanyika Dar es Salaam kwa kuandaliwa na Chadema, Januari 24. (Picha na Mpigapicha Maalum).

NUKUU



Ungwana ni kusaidiana katika shida zaidi, kwenye raha - mengi mabaya hujificha. Hivyo, ukitaka kutambua watu wako wa karibu na namna wanavyokupenda, basi watazame wanavyojitoa kwako wakati wa shida na utabaini nani ni nani - Msemo wa Kilatini.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

Ni zamu ya CCM kuandamana

Na Plato Hekimachius

YALIYOITWA maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), yamefanyika kwa amani na kumalizika.

Maandamano hayo yalifanyika Jumatano iliyopita – Januari 24 katika Jiji la Dar es Salaam. Yaliongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe.

Tumesikia ujumbe wao na dunia imewasikia. Watu wengi wameeleza na kuchambua mafunzo yaliyopatikana kutokana na maandanano hayo. Tafsiri nyingi zimetolewa na hilo siyo somo la makala yangu leo.

Kwa kuwa maandamano ya Chadema yalipingwa tangu kuandaliwa kwake, lakini bado yakafanyika, natamani waliokuwa wanayapinga waandamane pia kwa amani na kutuekeza sisi Watanzania agenda zao.

Kwa hiyo Chama Cha Mapinduzi (CCM), serikali, vyama 13 vya upinzani na umoja wa bodaboda, waandae maandamano na kutuandikia mabango ili tusome na kutafakari ujumbe wao pia.

Kwa kuwa walikuwa wanapinga agenda za maandamano ya Chadema, tunategemea watuletee mabango yenye agenda zilizo kinyume na za Chadema.

Watuambie kuwa gharama za maisha ziko chini. Sukari, mafuta, umeme na nauli za usafiri viko chini mno. Waiombe serikali iviongeze ili ijipatie kodi ya kutosha kufanya kazi za maendeleo.

CCM waingie barabarani waseme miswada ile mitatu isisitizwa kuwa hakuna haja ya tume huru ya uchaguzi, hakuna haja ya uchaguzi huru na wa haki.

Na kwamba madiwani, wabunge na rais wetu waachwe waendelee kutuletea maendeleo. Gharama za uchaguzi zipelekwe kwenye madawati na hospitali.

Wapendekeze kuwa muswada unaomhusu msajili wa vyama vya siasa



Maandamano ya Chadema

uongezewe makali ili kila chama kikabidhi ufunguo mmoja wa ofisi yao kwa msajili ili kila wakati awe anafika kusaini cheki na kukagua wasiofika kazini.

Maandamano ya CCM yaseme hali ya ajira kwa vijana ni nzuri sana na bima ya afya inahudumia watu vizuri. CCM impongeze Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendesha vizuri maridhiano ya kitaifa.

Zaidi pia Rais Samia apongezwe kwa kuwa maeneo mengi ya maendeleo yaliyokabidhiwa kwa wageni, kwa jina la wawekezaji, kwamba yanafanya kazi vizuri sana na sasa afikirie kubinafsisha na sehemu nyingine zisizofanya vizuri ili Tanzania ipate neema zaidi na watu wake kuishi kwa furaha kubwa.

Mwisho maandamano ya CCM yampongeze Katibu Mwenzi wake, Paul Makonda kwa kupenda maridhiano mpaka akatamani kwenda kulala kwa Mbowe.

Makonda pia apongezwe kwa kuwawajibisha watendaji wa serikali na kuwaita majukwaani mpaka suruali zinalowana.

Atiwe moyo ili hata waliompiteza Ben Saanane na waliompiga risasi Tundu Lissu, Makamu wa Mwenyekiti wa Chadema, atoe siku saba wawe wamepatikana na kufikishwa mahakamani.

CCM wakifanya hivi, wataeleweka, wataungwa mkono na kuchangia ukuaji wa demokrasia hapa nchini.

Kama CCM hawataki kuandamana wawaache wanaotaka kuandamana waandamane.

Habari

Anayepanga kuiba kura, atakufa – Lema

Na Tryruckia MFINANGA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Godbless Lema ametabiri kuwa yeyote anayepanga kuiba kura - kwenye uchaguzi ujao, hatafika kipindi cha kupiga kura, kwani atakufa.

Kwamba kupanga jambo la kudhulumu haki ya wengine, ni chukizo kwa Mungu, hivyo mwenye nia ya kupanga kuiba kura halali, atapoteza maisha kati ya sasa na mwishoni mwa mwaka ujao – 2025.

Tanzania itafanya uchaguzi wake wa viongozi wa serikali za mitaa – kupata madiwani, mwaka huu kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu Oktoba, 2025 - kwa rais na wabunge.

Lema, mbunge wa zamani wa Arusha Mjini aliweka hadharani maono yake hayo juzi wakati akihojiwa na mtangazaji Edwin Odemba wa runinga ya Star, katika kipindi cha Medani za Siasa, huku akibainisha kwamba atagombea ubunge wa jimbo aliloliongoza kwa miaka 10 hadi mwaka 2020.

Kiongozi huyo wa Chadema ambaye alikimbilia uhamishoni Canada wakati wa utawala wa Rais John Magufuli, alifumba fumbo ambalo linaweza kutafsirika kuwa ni; “kamwe mtu muovu hawezi kuachwa akamea, lazima atakufa kwa kura matendo yake yanaumiza idadi kubwa ya watu.”

Hii siyo mara ya kwanza kwa Lema, ambaye hukataa kujiita nabii, kutokana na kutabiri mambo ambayo hutokea. Kiongozi huyo aliwahi kutabiri kifo cha Rais John Magufuli katika mkutano wa hadhara.

Utabiri huo wa Lema ulimletea mgogoro na vyombo vya ulinzi na usalama.

Pambazuko linatambua kuwa madai ya wizi wa kura ama kutotangazwa kwa washindi halali wa uchaguzi, kimekuwa kilio cha Chadema, kama ilivyokuwa



Godbless Lema

kwa chama kingine cha upinzani, CUF – wakati huo kikiwa na nguvu kubwa, hasa Zanzibar.

Kwamba katika uchaguzi uliopita; 2015 wogombea ubunge wengi wa vyama hivyo walipokwa kura zao kwa wizi ambao ulikinufaisha Chama Cha Mapinduzi (CCM). Wanaotuhumiwa na vyama hivyo kufanya wizi huo ni wafuasi wa CCM, baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi na hata baadhi ya vyombo vya ulinzi.

Kilio kikubwa, manung'uniko na malalamiko ya Chadema kwa uchaguzi uliopita wa 2015, kilikuwa ni kuibwa kwa kura, lakini zaidi kutotangazwa kwa washindi halali, hasa kwa wogombea wake wa nafasi za ubunge.

Viongozi wa Chadema na wanaharakati waliokuwa wakifuatilia kwa karibu mchakato wa kupiga kura na kutangazwa kwa matokeo, wamekuwa wakiuita uchaguzi wa mwaka 2015, kuwa ni “uchafuzi-“ kutokana na kile kinachodaiwa kuwa ni vurugu katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Lema pia alitumia kipindi hicho kuwaeleza Watanzania na dunia kuwa maridhiano yaliyokuwa yakiendelea kati ya chama chake na CCM, yalikwamishwa na chama tawala kwa kutokuwa na dhamira ya dhati ya kusaidia kuondoa umasikini kwa Wananchi.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Marekani itatoa wapi uthubutu tena?

MIONGONI mwa habari zilizotawala duniani wiki iliyopita ni uamuzi wa Korti ya Kimataifa ya Haki (International Court of Justice) kuhusu kesi iliyowasilishwa kwake na Afrika Kusini dhidi ya Israeli.

Pamoja na tuhuma nyingine, Afrika Kusini iliishtaki Israeli kuwa inaendesha mauaji ya kimbari huko Gaza - Palestina.

Kabla ya uamuzi wa korti hiyo, kulikuwa na wasiwasi endapo haki ingetendeka hasa kwa vile mataifa makubwa duniani; Marekani, Uingereza, Ufaransa na Canada, yalijitokeza hadharani kuipinga kesi hiyo ya Afrika Kusini, huku mataifa hayo yakidai kuwa kinachofanywa na Israeli siyo mauaji ya kimbari, bali ni kutekeleza haki yake ya kujilinda.

Kadhalika, kutokana na muundo wa korti hiyo, ilidhaniwa kuwa huenda mataifa hayo makubwa yakawashinikiza majaji wanaotoka nchi hizo “waipendeleo Israeli”.

Hata hivyo, japo uamuzi wa korti hiyo haukutamba bayana kuwa Israeli inafanya mauaji ya kimbari, wala kuitaka nchi hiyo iache mashambulizi yake huko Gaza, kwa kiasi kikubwa, korti hiyo ilikubaliana na hoja zilizowasilishwa na Afrika Kusini.

Lakini, kila mwenye uelewa kuhusu vita hiyo ya Gaza na pengine siasa za kimataifa kwa ujumla, atakuwa anafahamu kuwa haikutarajiwa kwamba uamuzi wa korti hiyo ungeweza kubadili chochote.

Kwa bahati mbaya – au pengine kwa makusudi – mataifa kama Marekani na Uingereza ambayo kwa miaka mingi yamejipachika wadhifa wa “askari wa maadili ulimwenguni,” yamekuwa ndumilakuwili ambapo “haki” ni kwa mujibu wa maslahi yao tu na siyo ya kila nchi.

Licha ya mataifa hayo kuipinga Afrika



Rais wa Marekani - Joe Biden

Kusini kuhusu mashtaka yake dhidi ya Israeli, mara baada ya uamuzi wa ICJ, mataifa hayo yakachukua hatua isiyo ya kibinadamu ya kusitisha michango yake kwa shirika la Umoja wa Mataifa la Misaada kwa Palestina (Unrwa), kufuatia tuhuma kuwa watumishi 12 wa shirika hilo walishirikiana na kikundi cha Hamas.

Hatua hiyo ilifuatia mataifa hayo makubwa kutoafikiana na uamuzi wa ICJ ambao pamoja na mambo mengine, umetaka Israeli kuhakikisha inalinda uhai wa watu wasio na hatia huko Gaza.

Kwa Marekani, Uingereza na mataifa mengine makubwa, kuikumbatia Israeli ilhali idadi ya watu waliouawa huko Gaza ikizidi vifo 26,000, ni dhahiri kuwa mfumo wa haki kimataifa ambao siyo tu umeingia doa, bali itayawia vigumu mataifa hayo makubwa kuwa na uthubutu wa kukemea ukiukwaji wa haki duniani pengine popote unapoweza kutokea kwa kuwa tayari yameharibu taswira zake.

Hivi kukitokea mauaji mengine ya idadi kubwa ya watu, Marekani, Uingereza na washirika wao wengine watakuwa na uthubutu wa kusimama na kukemea wakati wameonesha kabisa wanaikumbatia Israel ambayo ni dhahiri, inahusika na mauaji ya kimbari dhidi ya Wapalestina?

Temblelea hapa kupata zaidi: https://instagram.com/evarist_chahali

Habari

Vitalu 24 vya mafuta vyathibitika Tanzania

Na Mwandishi WETU

NEEEMA ya mafuta katika Tanzania inazidi kudhihiri baada ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (Pura), kutangaza kwamba iko mbioni “kuachia vitalu 24 vya mafuta kwa wawekezaji.”

Vitalu hivyo, vitatangazwa hivi karibuni kwa wawekezaji wa ndani na nje ili waweze kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kuthibitisha kiasi cha mafuta kinachopatikana.

Mkurugenzi Mkuu wa Pura, Mhandisi Charles Sangweni amebainisha hayo juzi – Jumamosi wakati wa mkutano wa pili wa Baraza la Wafanyakazi Pura, Mjini Morogoro na kubainisha kuwa hivi sasa anatafutwa mtaalamu wa kubaini mipaka halisi ya kisheria ya vitalu hivyo kabla ya kutangazwa kwa wawekezaji.

“Kazi hii ya kuweka mipaka, inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita kuanzia sasa, na baada ya hapo, wataalamu wetu watakuwa na vikao mbalimbali, ndani na nje ya nchi ili kueleza uwepo wa vitalu hivyo,” ameingiza Mhandisi Sangweni.

Mhandisi huyo amesema kuwa sehemu za mikoja Singida, Tabora na Manyara, zimeonesha kuwa na akiba kubwa ya mafuta na gesi, hivyo yapo maeneo ambayo serikali – kupitia Pura, itayatenga kwa ajili ya uchunguzi na upembuzi yakinifu kubaini kuwepo kwa kiasi cha nishati hizo.

Pambazuko limeelezwa kuwa baada ya maeneo hayo kubainishwa na kutangazwa rasmi, wenye maeneo hayo watalipwa fidia stahiki ili kutoa nafasi kwa shughuli zaidi za kutafuta mafuta na gesi kuendelea.

Akizungumza katika mkutano huo, mgeni rasmi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Selemani Mbuttuka aliwaagiza Pura kuwa makini katika kazi zao na kuhakikisha kila hatua ya utendaji wao inafata sheria za nchi.

Alihimiza Pura kuingeza bidii kusomesha watendaji wake, ili waendane



Mhandisi Charles Sangweni

na kasi ya ukuaji wa sekta ya uziduaji, ambayo inabadilika mara nyingi – na kwa muda mfupi kutokana na kukomaa kwa teknolojia.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Mhandisi Sangweni alisema tangu mamlaka hiyo ianze kufanya vikao vya baraza, ushirikishwaji wa wafanyakazi katika masuala mbalimbali yanayohusu Pura umeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mbuttuka akizungumza na wafanyakazi hao alisema kuwa miongoni mwa majukumu ya msingi ya baraza ni kuhakikisha kuwa haki na wajibu wa mwajiri na mtumishi vinapewa kipaumbele katika utekezaji wa majukumu.

“Daima tukumbuke kuwa ili utumishi wa umma uweze kuheshimika, ni wajibu wetu tukiwa watumishi kufanya kilicho sahihi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.” Aliongeza naibu huyo.

Moja ya majukumu makubwa ya Pura ni kuishauri serikali katika shughuli zote za uziduaji, hasa mafuta na gesi na kuchunguza na kubaini uwepo wa nishati hizo, kuangalia na kupima ubora wake na zaidi kufuatilia kazi zote za wawekezaji katika sekta ya uziduaji. Pura ilianzishwa rasmi mwaka 2015.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

ACT-Wazalendo na fahari ya 'Cossovo'

CHAMA cha siasa cha Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo) kiliposajiliwa Mei 2014, uongozi wa kina Samson Mwigamba na Lucas Limbu kilikuwa kikijulikana kwa jina la ACT-Tanzania.

Nguvu ya wakati ule haikuwa kubwa ikilinganisha na sasa baada ya baada ya mwanasiasa na mbunge wa zamani wa Kigoma Mjini, Zitto Zubeir Kabwe alipojiunga nayo mwaka mmoja baadaye - Machi 2015.

Ujio wa mwanasiasa huyu ambaye alitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), uliondoa neno Tanzania na badala yake likawekwa Wazalendo.

Lakini, Machi 18, 2019 mwelekeo mpya wa kisiasa Tanzania ukaendelea kunoga baada ya aliyekuwa katibu mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Maalim Seif Shariff Hamad kujiunga na ACT-Wazalendo.

Maalim Seif (sasa marehemu), alichukua hatua hiyo muda mfupi baada ya uamuzi wa Mahakama Kuu kumpa ushindi wa kuendelea na jukumu la uwenyekiti wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, baada ya mvutano kati yao.

Kunoga kwa mwelekeo huo mpya, hasa kulichochea na mwanasiasa huyo mwenye ushawishi katika siasa za visiwani Zanzibar kuhama na baadhi ya wanasiasa waandamizi waliokuwa wakimuunga mkono.

Kujiondoa kwa Maalim Seif katika chama alichodumu nacho kwa zaidi ya miongo minne, kulitarajia kuandika historia mpya katika medani za siasa Zanzibar, na hili lilithibitika katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ambapo ACT-Wazalendo kilifanikiwa kuingia katika serikali ya Umoja wa Kitaifa chini ya kauli-mbiu yao 'Shusha tanga, pandisha tanga'.

Ingawa Maalim Seif amefariki dunia, lakini 'mbegu' njema ya wanasiasa vijana



Zitto Kabwe - Kiongozi Mkuu wa ACT_Wazalendo

aliyoipanda, ingalipo na pengine ndiyo maana ACT-Wazalendo leo imefanikiwa kuweka uongozi wa matawi mpaka vijijini.

Kwa namna nilivyoshuhudia wanachama wakichaguana kwa shangwe katika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye mikoa ya Morogoro, Njombe na Dodoma chini ya usimamizi wake, Aoubakar Salum Kitogo, wafuasi wake wamenikumbusha hamasa ya matawi maarufu ya Taleban, Chechnya na Cossovo ya jijini Dar es Salaam.

Cossovo, Chechnya na Taleban ni baadhi ya matawi maarufu ya CUF yaliyojipambanua katika kile walichokiita kudai haki sawa kwa wote, mithili ya nchi hizo zilizokuwa katika muungano wa iliyokuwa Urusi (USSR).

Enzi zile CUF haikuhitaji taarabu, bongo fleva wala singeli zitumbuize ndipo wafuasi waja, hapana, wanachama tu kutoka katika matawi haya peke yao walikuwa "wanatosha."

Ikumbukwe kuwa uhai wa chama unategemea uwepo wa matawi imara yenye wakareketwa, wafurukutwa na wafia chama wenye kujitua kwa ajili ya chama chao.

Sasa ni wakati wa kila chama kuwa na matawi vijijini yenye hamasa kubwa kama ilivyokuwa kwa Taleban, Chenchnya na Cosovo.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 au Barua pepe:mtagaluka@gmail.com

Jicho la Tai

Mpango arejeshe ujira wa Novemba

IMEKUWA ugomvi usioisha na hata mwandishi wa Tai kutishwa kufukuzwa kazi, eti kwa kuwa hajafanya kazi aliyotumwa na mwajiri wake.

Wiki iliyopita, mwandishi wa Tai aligoma kuandika yale aliyotakiwa kuyaweka gazetini na mwajiri, kwa kuwa alishikilia msimamo wake kwamba – anadhani hatatenda haki kwa kukosa ushahidi wa kuandika alichotakiwa.

Hakika ulikuwa ugomvi mkubwa na kwa hasira, Tai alifungasha virago na kwenda Morogoro kupumzika, akidai kwamba mwandishi wake amejenga kiburi kwa kuwa labda hajaongezwa mshahara kwa miezi kadhaa sasa.

Hasira za Tai zilitokana na nongwa yake ya kutaka kuandikwa kwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Philip Isdor Mpango.

Kwamba zipo taarifa kuwa mwezi mzima wa Novemba, mwaka jana, kiongozi huyo hakuonekana ofisini na wala hakukuwa na taarifa zozote rasmi kwa umma - za wapi alikuwa na alikuwa akifanya nini.

Ugomvi wa Tai ukawa hapo; mwandishi wake akashauri ni vyema kuendelea kusubiri ili zitoke ama zipatikane taarifa rasmi za wapi alikuwepo Dkt. Mpango.

Hata hivyo, jana ghafla Tai akarejea Dar es Salaam, akiwa na bashasha la furaha iliyothibitika kujaa kapu, tena lililosukwasukwa nusura ya kumwaga kilichomo.

Mwandishi wake akauliza, kulikoni? Tai akajibu, nimekuletea sasa uthibitisho kwamba Dkt. Mpango hakuwa kazini mwezi Novemba, 2023 na hakukuwa na taarifa zozote, sasa ameupata ushahidi, hivyo kumwamuru mwandishi wake aandike.

Aandike nini? Eti aweke maandishi ndani ya Pambazuko ya kumtaka Dkt. Mpango kurejesha ‘mpango’ – kwa maana ya mshahara ama kwa jina jingine, ujira wote wa Novemba kwa kuwa hakufanya kazi.



Daktari Philip Isdor Mpango

Mwandishi akashikwa na butwaa, ushahidi gani anao huyu Tai, au anazeeka vibaya? Au hamtakii mema mwandishi – kwamba anataka aanze kusumbuana na watu bila sababu za msingi.

Wakati mwandishi anaendelea kushangaa, mara – pwaa! Tai akadondosha picha zinazomuonesha Dkt. Mpango akiwa katika pilikapilika za kupokea wageni, kuaga na kushiriki katika kazi za Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM).

Picha za kwanza zikionekana zimepigwa Januari 24, jijini Dar es Salaam, Dkt. Mpango – akiwa na siha njema, anaagana na Makamu wa Rais wa Cuba, Salvador Valdés Mesa.

Nyingine picha – za jana tu, zinaonekana makamu wetu akiwasili Kigoma na kupokewa na viongozi wa UVCCM.

Tai, huku akiwa amelegeza mbawa zake, alisema – “sasa kazi kwako, iweje kiongozi wetu, tena tumemwajiri, ana timu ya wapiga picha, asiwe na picha hata moja akiwa kazini Novemba, haiwezekani!”

Tai akaendelea; “Huyu mwajiriwa wetu hakuwa kazini kwa mwezi wote wa Novemba, 2023. Arudishe mshahara tuupangie kazi nyingine.”

Tai akaondoka zake. Sasa mwandishi anajuliza, aandike ama asiandike!

Maono ya Rais Museveni yang'ara

Na Mwandishi WETU

IJUMAA iliyopita, Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda, aliadhimisha miaka 38 ya kuiongoza Uganda kuanza safari ya kuleta maendeleo yanayoonekana sasa.

Katika miaka hiyo, Museveni aliongoza jeshi la National Resistance Army (NRA) kumuondoa madarakani aliyekuwa kiongozi wa nane wa nchi hiyo, Tito Okello Lutwa.

Hivi sasa akiwa na zaidi ya miongo mitatu ya utawala wake, Rais Museveni ameshuhudia Uganda ikipiga hatua kwenye nyanja tofauti, zikiwemo za kijamii, kisiasa na uchumi.

“Ushindi wa NRM wa tarehe 26 Januari, 1986, ulikuwa ni kiashiria cha uimara wa watu wetu na uwezo wao wa kukabiliana na changamoto mbalimbali,” anasema Museveni katika hotuba yake kwa taifa aliyotoa siku ya Alhamisi, siku moja kabla ya kilele.

Kiongozi huyo mwenye bashasha nyingi ana amini kuwa Uganda inaendelea kuwa imara katika kukabiliana na changamoto kadhaa wa kadha.

Usalama ni mojawapo ya changamoto hizi, hasa za mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kikundi kwa kikundi cha ADF.

Mwaka uliopita waasi hao waliripotiwa kuwashambulia na kuwaua watalii kutoka Uingereza za Afrika Kusini, akiwemo dereva wao mwenye asili ya Uganda.

“Usalama wa nchi unaendelea kuwa imara na serikali inaboresha zaidi uwezo wake wa kiusalama na miundombinu ya kisasa ili kugundua matukio ya kigaidi kabla hayajatokea,” Museveni anasema.

Kiongozi huyo anasisitiza kuwa Uganda imeboresha na kuongeza uwezo wake wa kupeleleza na kufuatilia viashiria vya matukio hatarishi ili kuhakikisha kwamba Waganda na watu wengine wanaendelea kubaki salama.

“Tumeboresha sana uwezo wetu wa upelelezi na ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba Waganda na wageni wetu



Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda,

wanaokuja hapa wako salama,” Museveni anaongeza.

Ukuaji wa Uchumi

Museveni amewahakikishia wananchi wake kuwa uchumi wa nchi yao unaendelea kukua, licha ya changamoto kama athari za mabadiliko ya tabia nchi kwenye kilimo na miundombinu kutokana na mafuriko.

Changamoto zingine ni mzozo unaoendelea Ulaya Mashariki, ambao umesababisha bei ya bidhaa muhimu kama vile mafuta kupanda katika siku za hivi karibuni.

“Uchumi wetu ulikua hadi kufikia dola za Marekani bilioni 49.5 katika mwaka wa fedha 2022/2023, kutoka dola bilioni 45.6 zilizopatikana mwaka wa fedha 2021/22,” anafafanua.

Kwa sasa, Uganda inatazamia kupata maendeleo zaidi ya kiuchumi, kwa miaka ijayo.

“Uchumi utakua kutoka thamani yake ya sasa ya dola za Marekani bilioni 48 kwa mwaka wa fedha 2022/23 hadi dola bilioni 55 kufikia mwisho wa mwaka wa fedha huu na kwenda mbali zaidi kufikia dola bilioni 60 katika mwaka wa fedha 2024/25,” anasema Rais Museveni.

Uhusiano na DRC

Rais Museveni amesema Uganda inapanga na kuhakikisha kuwa na ujirani mwema, hasa na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Sehemu kubwa ya taarifa hii imepatikana TRT – Afrika.

Habari**Biashara Ikulu Z'Bar yavuruga uongozi**

Na Mwandishi WETU,
Zanzibar

KUFANYIKA kwa biashara ndani ya Ikulu ya Zanzibar, kumeelezwa kuwa chanzo kikuu cha kuparaganyika kwa maadili ya uongozi.

Ni kutokana na kumomonyoka kwa misingi ya uongozi na utawala bora, baadhi ya watendaji wakuu wa Ikulu, wamekuwa wakiingilia dhamana na uamuzi wa wasaidizi – hasa mawaziri, wa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Pambazuko limeeleza kinagaubaga.

Msingi huo wa kuingilia uamuzi wa mawaziri, ndiyo sababu kuu ya kujiuzulu ghafla kwa aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohammed Said.

Simai alitangaza kujiondoa katika nafasi yake Jumatano – Januari 24, usiku wa saa 6:42, baada ya kujirekodi kwa simu na kusambaza video yake kupitia vyombo vya habari, huku akieleza sababu ya kufanya hivyo ni “kutokuwepo kwa mazingira rafiki ya kufanya kazi.”

Kwanini Simai akurupuke usiku mkubwa kutangaza kuachia ngazi? Ndiyo swali linalogonga vichwa vya wengi, lakini Pambazuko limeeleza kuwa alifanya hivyo ili kuuwahi uamuzi wa Rais Dkt. Mwinyi wa kufanya mabadiliko ya baraza la mawaziri, ambayo yalikuwa yanamuengua.

Simai ni mfanyabiashara na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Jimbo la Tunguu, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alipoulizwa na Pambazuko endapo alipata fununu za kuenguliwa, Simai hakukataa wala kukubali, bali alishikilia msimamo wake kwamba; “nimeamua kuondoka kwa kuwa mazingira ya kazi siyo rafiki.”

Je, lini yalianza kutokuwa rafiki? Simai hakupenda kujibu swali hilo, bali akasema; “mambo hubadilika.”



Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Hakika Ikulu ya Rais Dkt. Mwinyi iliutangazia umma kuwepo kwa mabadiliko ya baraza la mawaziri juzi - Jumamosi, Januari 27.

Kujiondoa kwenye nafasi ya uwaziri, tena akiwahi Ikulu kabla ya uamuzi, huenda ndiyo kumehitimisha urafiki wa karibu wa Rais Mwinyi na Simai ambao tangu wakiwa vijana, walikuwa na ukaribu kutokana na baba zao kuwa mabalози.

Baba yake Simai, Mohammed Said aliwahi kuwa ofisa ubalози na baadaye kuukwaa ubalози na kuhudumu katika nchi za India na Misri, maeneo ambayo baba wa Rais Dkt Mwinyi, Ali Hassan Mwinyi alihudumu.

Kufanyika biashara Ikulu

Mbali na kuwepo kwa mparaganyiko wa Ikulu kuingilia majukumu na uamuzi wa mawaziri, kuwepo kwa madai ya kufanyika biashara Ikulu ya Zanzibar, ni sababu nyingine ya Simai kuamua kuachia ngazi.

Pambazuko limeeleza kuwepo kwa familia au marafiki wa viongozi kadhaa wa Ikulu kufanya biashara ya vileo, wakati huohuo, Simai akiwa ana familia inayofanya biashara ya namna hiyohiyo.

Katika siku za karibuni, waliokuwa wakifanya biashara ya kuagiza vileo, walinyang'anywa leseni zao na Bodi ya Vileo Zanzibar na kupewa watu wengine, ambao kutokana na kukosa uzoefu,

Biashara Ikulu Z'Bar yavuruga uongozi

Inatoka Uk. 12

walikwama kusambaza vinywaji hivyo kwa muda, hivyo kusababisha upungufu wake.

Hatua ya waagizaji wazoefu kunyang'anywa leseni, kulimkasirisha Simai, hasa ikizingatiwa kuwa utalii ndiyo injini ya kukusanya mapato ya Serikali ya Zanzibar.

Pambazuko limeelezwa kuwa baada ya hali hiyo, Simai aliwasilisha hoja yake Ikulu kwamba wafanyabiashara wazoefu, warudishiwe leseni zao, lakini aligonga mwamba.

Pambazuko limeambiwa kuwa Simai aliwaeleza Bodi ya Vileo Zanzibar kurejesha leseni za wafanyabiashara wazoefu, lakini alijibiwa na mmoja wa viongozi wa bodi hiyo kuwa; "hatuwezi, kwani waliopo hawa wapya, wameletwa kwa maelekezo kutoka Ikulu."

Kampuni za kuagiza na kusambaza vileo Zanzibar ambazo zimekuwa na uzoefu katika biashara hiyo ni pamoja na ZMMI, Scoch na One Stop.

Baada ya kuwepo kwa malalamiko ya wenye hoteli za kitalii na migahawa kuhusu kuwepo kwa uhaba wa vileo, Simai akiwa bado waziri mwenye dhamana, aliitisha mkutano wa wamiliki wa biashara hiyo na kubaini kukosekana kwa uzoefu wa kampuni mpya zilizopewa kandarasi kuagiza vileo.

"Tumeona uamuzi wa Bodi ya Vileo Zanzibar imewaondosha wale waliokuwa wanahusika zaidi kama ZMMI, Scoch na One Stop, nimeanza kuona athari, hoteli nyingi wameanza kukosa huduma ya vinywaji baada ya bodi kufanya uamuzi huo, niwaombe wawekezaji waendeleo kuwa wavumilivu wakati huu ikitazamwa namna ya kutatua jambo hili," alisema Simai, ambaye alipenda kujitanabaisha kuwa ni "baba wa mahoteli na migahawa Zanzibar.

Dalili za kuondoka ama kuondoshwa



Simai Mohammed Said.

kwa Simai katika nafasi yake kunadaiwa kuonekana mapema, hasa baada ya kutokea mvutano kuhusu kuagiza vileo ndani ya Zanzibar.

"Nakuhakikishia huyu kijana alijua wakati wowote ataondoshwa mamlakani. Kitendo chake cha kupeleka ombi la kujiuzulu, ni kumuwahi mshemiwa rais. Na hayuko peke yake," alisema ofisa mwandamizi katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, mjini Zanzibar.

Kada huyo wa CCM ambaye alizungumza na Pambazuko kwa sharti la kutotajwa jina gazetini, alisema hata Jamal, naye alikuwa amekalia "kuti kavu," licha ya kuwa rafiki mkubwa wa Rais Dkt. Mwinyi.

Anadai kuwa sababu ya kuondoshwa kwa Jamal, huenda ni ileile aliyoitaja Simai wakati akitangaza kuachia ngazi; "kutokuwepo mazingira rafiki ya kufanya kazi, hasa na wakubwa walioko Ikulu."

CCM Zanzibar kubaki imara?

Baada ya kuwepo kwa mabadiliko ya baraza la mawaziri, na kuondolewa kwa baadhi ya wanasiasa wakongwe, wachambuzi wa siasa katika visiwa hivyo, wanahoji, endapo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kitaendelea kuwa imara Zanzibar.

Mabadiliko haya ya baraza la mawaziri yaliyomuengua pia swahiba mwingine wa Rais Dkt. Mwinyi, Jamal Kassim Ali, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, yanajenga hofu ya

Habari

Biashara Ikulu Z'Bar yavuruga uongozi

Inatoka Uk. 13

uimara na mshikamano wa chama hicho tawala.

Hatua ya kujiuzulu ghafla kwa Simai aliyekuwa akishika moja ya wizara muhimu na mhimili wa kuchagiza kasi ya ukuaji wa uchumi kutokana na sekta ya utalii kuwa sekta kiongozi katika kuipatia Zanzibar mapato makubwa ya fedha za kigeni, ilijibiwa haraka na Rais kwa kupangua baraza lake ikiwa ni miaka miwili sasa tangu alipofanya mabadiliko madogo ya kwanza Machi 8, 2022.

Kutokana na mabadiliko yaliyofanywa, nafasi ya Simai sasa inashikwa na Mudrick Suleiman Soraga.

Kabla ya hapo, Soraga alikuwa Wizara ya Uchumi, Kazi na Uwekezaji.

Ismail Khamis Kheri, mchambuzi wa masuala ya siasa za Zanzibar, amesema - “maslahi binafsi na mgongano wa maslahi” kati ya mamlaka ya juu ya uongozi na wateuliwa wa Rais ni chanzo cha kutetereka kwa uamuzi wa mawaziri, hivyo kuna hatari ya “kukinyong’onyesha” chama cha CCM.

Katika mabadiliko mapya, Rais Dk. Mwinyi pia amemteua Ali Suleiman Ameir, aliyekuwa naibu waziri hapo chini ya Jamal, kupanda ngazi na kumpa dhamana ambayo yeye alikuwa ni msaidizi.

Ameir ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Pangawe, Wilaya ya Magharibi B, Unguja, ambaye kabla ya kuingia katika siasa na kugombea uwakilishi wakati wa uchaguzi mkuu wa



Mudrick Suleiman Soraga.

mwaka 2020, alikuwa ofisa mwandamizi katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Wote Simai, Soraga, Jamal na Ameir ni wanachama wa CCM, chama ambacho kutokana na mijadala iliyoopo katika jamii kwa sasa, inaonekana kinapita kwenye joto kali la “kupigania kuendelea kukubalika.”

Ni katika muktadha huo, zinapatikana taarifa ndani ya CCM, zikisema mabadiliko hayo yaliyomuweka kando Jamal ambaye ni swahiba mkubwa wa Rais Dkt. Mwinyi, yanazidi kudhoofisha mshikamano kichama, na kiutendaji kwenye serikali.

Haya yakichanganyika na malalamkiko ya muda mrefu ya namna uamuzi wa shughuli za uwekezaji yanavyotatizwa na uhusiano wa karibu mno wa Rais na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwekezaji Vitegauchumi Zanzibar {ZIPA}, Shariff Shariff, yanatia shaka kama ukusanyaji wa mapato utaendelea kuwa wa kasi.

“Kwenye hili ninadhani panahitajika uangalifu mkubwa kwa sababu Jamal alikuwa mkali kwenye suala la usimamizi wa mapato huku Simai akiwa rafiki muhimu kikazi na wafanyabiashara waliofika kutaka kuwekeza katika sekta ya utalii,” amesema mmoja wa wakurugenzi kwenye wizara ya utalii.



Hoteli ya Zanzibar Beach - moja ya vivutio vya watalii visiwani



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi


Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Kitabu

Bei sh 45,000/=
DAR: Free delivery
Mikoani: delivery
sh 5,000/=



M-Pesa 0767-340-975
jina Anna



Instagram: @evarist_chahali

Twitter: @chahali

TikTok: @j.a.s.u.s.i

www.baruayachahali.com

CCM na utawala uliofitinika

Na Mwandishi WETU

UKIWA mfuatiliaji mzuri wa siasa za Tanzania kwa muda mrefu, unaweza kupata picha kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM), hakijatulia; bado kinaweweseka. Hakijajua kinasimama wapi.

Ingawa ni chama tawala wakati fulani hufanya mambo ambayo unaweza kudhani hakijui kinafanya nini na kwa sababu gani. Wakati mwingine unaweza kudhani kuwa kinawajaribu Watanzania.

Fikiria kwa mfano, kurejea kwenye uongozi kwa kwa Paul Makonda, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM hivi sasa. Huyu ni mtu ambaye aliwahi kushika nafasi kadhaa za uongozi awali, akiacha nyuma yake mlolongo wa tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka akiwa kiongozi.

Ni kijana mwenye akili, lakini aina yake ya uongozi ilimfanya asipendwe sana na watu wengi wakiamini kuwa hakuwa mpenda watu.

Marekani ilifikia hatua ya kumpiga marufuku kuingia nchini humo kutokana na tuhuma zilizohusiana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Zuo hilo halijawahi kuondolewa hadi leo.

Aliondoka kwenye sura za uongozi baada ya kushindwa wakati alipowania nafasi ya kuteuliwa kugombea ubunge katika Jimbo la Kigamboni. Alikwenda kwenye kinyang'anyiro hicho akiacha nafasi ya ukuu wa mkoa ambayo alikuwa anaishikilia.

Ingawa tuhuma haziwezi kusababisha mtu anyimwe uongozi, lakini katika uongozi uliotukuka, kutuhumiwa ni moja ya jambo ambalo linaweza kumfanya kiongozi mnyoofu kuachia madaraka yake kama alivyofanya aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo.

Lakini, licha ya tuhuma lukuki dhiid yake, Makonda akarejeshwa kwenye uongozi ndani ya CCM, tena kwenye



Paul Makonda, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM

dhamana kubwa ya ukatibu wa itikadi na uenezi, nafasi ambayo inampa fursa ya kuwa mjumbe wa sekretarieti ya chama hicho tawala.

Makonda alirejesha CCM wakati Chongolo akiwa Katibu Mkuu. Ni Chongolo huyohuyo ambaye akiwa Mkuu wa Wilaya na Kinondoni, Dar es Salaam, alinyamazishwa kwa namna ya kudhalilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati huo, Paul Makonda.

Ilipotangazwa tu kuwa Makonda anarejeshwa CCM huku Chongolo akiwa bosi wake, baadhi ya watu wakatabiri kuwa mmoja kati ya hao wawili, ataondoka kwenye nafasi yake baada ya muda mfupi.

Utabiri huo ulitimia kwani Chongolo alijiuzulu nafasi yake wiki chache tu baada ya Makonda kushika wadhifa wake huo mpya.

Chongolo alijiuzulu kwa namna ambayo inafikirisha kidogo. Zilizushwa tuhuma kwenye mitandao ya kijamii zikimhusisha na masuala ambayo ni kinyume na maadili ya uongozi.

Kwa kuwa Chongolo ni mtu nyoofu, tuhuma hizo, hata kabla hazijachunguzwa, akaamua kujiuzulu.

Wakati Makonda akitangaza uamuzi wa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia

Makala**CCM na utawala uliofitinika****Inatoka Uk. 17**

Suluhu Hassan kukubali kujiuzulu kwa Chongolo, alisema kuwa imeundwa timu ya kuchunguza kadhia hiyo na uzushi dhidi ya Chongolo.

Hadi leo haijaezwa timu hiyo imefikia wapi katika uchunguzi wake, lakini tunachofahamu kwa uhakika ni kuwa CCM imemteua Dk. Emmanuel Nchimbi kurithi nafasi ya Chongolo.

Wakati Makonda anateuliwa kushika dhamana aliyonayo sasa, chini ya Chongolo, kuna baadhi ya watu walijiuliza ni nini kimemsukuma mwenyekiti wa chama hicho kufanya uteuzi huo?

Hawa walikuwa wakirejea sekeseke lilimkumba Chongolo akiwa chini ya ubosi wa Makonda. Sasa Makonda anakuja kuwa chini ya boshi Chongolo, hali itakuwaje?

Makonda alipoingia kwenye nafasi yake mpya akaanza kazi zake kwa mbwembwe za aina yake. Akaandaa ziara akipita mikoa kadhaa na huko akawa anawakaripia viongozi wa serikali na watendaji wengine kwa mgongo wa chama tawala.

Akitoa amri kwa viongozi wa serikali na watendaji wengine akisema kuwa chama ndicho wanachokitumikia na ndicho kilichoshika hatamu za uongozi.

Ni kweli chama ndicho chenye hataumu za uongozi, lakini kila mmoja anafahamu kuwa yanapotolewa maagizo na maelekezo hata na chama chenyewe, basi kuna aina fulani ya ustaarabu na heshima ya kuwasilisha maagizo na maelekezo hayo.

Lakini, msamiati huo inaelekea haupo kwa Makonda, kwani maagizo na amri zake anazitoa kwa namna ileile tuliyoizoea kwake, ya kudhalilisha.

Mara baada ya Dk. Nchimbi kuingia ofisini, Makonda akawa ameandaa ziara nyingine akaanza zile mbwembwe zake za kutoa amri na maagizo kwa viongozi wa serikali na watendaji.

**Makamu Mwenyekiti CCM- Abdulrahman Kinana**

Wakati akipokelewa Dodoma, Dk. Nchimbi akatoa kauli akiwataka viongozi wa CCM kutowakaripia viongozi wa serikali na watendaji wakati wanapokutana nao kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Dk. Nchimbi hakumtaja kiongozi yeyote wa CCM wakati anatoa maelekezo hayo, lakini inawezekana kabisa kuwa wakati yeye akizungumzi hayo Dodoma, Makonda akiwa huko ziarani alikuwa anatoa amri na maagizo kwa viongozi wa serikali na watendaji.

Hata hivyo, ukiachana na hawa wanaohisi, ipo kauli ya uhakika ambayo imetolewa na Makonda mwenyewe, akiwa katika ziara zake huko mikoa ya kaskazini.

Amesikika akitamka kuwa angeteuliwa kuwa mwenezi wakati wa uongozi wa Rais John Magufuli (sasa marehemu), basi wapinzani wangenyooka.

Ukirejea jinsi utawala wa Magufuli ulivyokuwa, mtu unapata woga. Sasa ukikutana na mtu ambaye anatamani kuwa mmoja wa viongozi katika utawala huo, sidhani kama utashindwa kupata woga, tena mtu huyo akisisitiza kuwa kama angewepo kwenye utawala ule, basi kuna watu wangenyooka!

Haya yote yanatokea ndani ya CCM ambapo tulitarajia kuwe na umoja na mshikamano, lakini kinachoonekana kwa kiasi fulani ni kusema kimafumbo na kukaripiana! Ni kama utawala uliofitinika juu yake chenyewe.

Kenya bado mwamba kwenye riadha

Na Mwandishi WETU

INAFAHAMIKA sasa, kwamba riadha nyumbani kwake ni Kenya.

Hali hiyo imethibitika jana tena, baada ya mwanariadha wa nchi hiyo ya Afrika Mashariki, Sammy Kitwara kuibuka mshindi wa kwanza katika mbio za Marrakech Marathon.

Kutokana na ushindi huo, Sammy amejizolea kitita cha zaidi ya Shilingi za Tanzania – milioni 25 (sawa na Shilingi ya Kenya – milioni 1.6).

Mashindano hayo yaliyojumuisha washindani wengi kutoka nchi mbalimbali duniani, yalikuwa kivutio kikubwa kwa wananchi wa Morocco – nchi kulikofanyika mbio hizo za marathoni, na wageni wengine.

Washiriki walikuwa 12, 000 wengi wakiwa na majina makubwa na uzoefu katika mbio hizo.

Sammy alikamilisha mbio hizo za kilomita 42 kwa saa 2:07:53 akifuatiwa kwa karibu na Wamoroco; Omar Ait Chitachen na Mustapha Houdadi kwa 2:08:43 na 2:09:36, mtawalia.

Nambari mbili na tatu walitia kibindoni Shilingi za Kenya milioni 1.1 na 650, 596, mtawalia.

Nao Wakenya wengine; Bravin Kiprof na Vincent Kipkorir wameshika nafasi ya kwanza nay a pili katika mbio za kilomita 21 za Sevilla kwa dakika 59:21 na 59:48 nchini Hispania, mtawalia.

Mwitaliano Iliass Aouani alifunga tatu-bora kwa saa 1:01:32.


Washindi hao watatu wa mbio za Seville, waliambulia Shilingi za Kenya - 176, 693; Sh132, 520 na 88, 346, mtawalia.

Wakenya pia walitawala mbio za Buriram Marathon nchini Thailand mnamo Januari 27, 2024.

Wakimbiaji wengine Sharon Chelimo (2:27:59), Caroline Jepchirchir (2:30:11) na Sheila Jepakosgei (2:32:11) walishika nafasi tatu za kwanza kwa pande wa wanawake.


Mathew Samperu (2:09:54), John Mwangangi (2:11:07) na Geoffrey Birgen (2:11:22) walifuatana katika nafasi tatu za kwanza upande wa wanaume, mtawalia.

Wakimbiaji hao watatu wa kwanza katika mbio hizo za kilomita 42 mjini Buriram watapokea tuzo ya Shilingi za Kenya milioni 7.3; milioni 3.2 na milioni milioni 1.6 kabla ya kutozwa ushuru, mtawalia.



Sammy Kitwara

Mbwembwe za Makonda...



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda anaendelea na ziara ya kukiimarisha chama chake kwa staili mpya ya kupokelewa na tingatinga. Hapa akiwasili mjini Kahama, Shinyanga juzi. (Picha kutoka mitandao ya chama hicho).

GAZETI hili lilianshwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaandeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

